JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA

# TANGAZO

## UUZAJI WA MAGOGO YA MTI WA MKURUNGU KWA NJIA YA MNADA KATIKA ENEO LA BANDARI YA NCHI KAVU – UBUNGO, DAR ES SALAAM

1. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) utauza magogo vipande 18,489 ya mti wa Mkurungu (*Pterocarpus Tinctorius*) yenye jumla ya meta za ujazo **1,357.026** iliyopo katika eneo la Bandari ya Nchi Kavu – Ubungo, Dar es Salaam. Magogo hayo yaliyopimwa ujazo katika makontena 59 yatauzwa kwa mnada kwa kuzingatia Kanuni ya 31 (ii) ya Kanuni za Sheria ya Misitu za Mwaka 2004. Magogo hayo ya Mkurungu yatauzwa mahali yalipohifadhiwa na jinsi yalivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo.

2. Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika eneo la **Bandari ya Nchi Kavu - Ubungo**. Mnada utafanyika siku ya **Jumatatu** ya tarehe **29 Machi, 2021** saa **4:30 asubuhi**.

3. Mnunuzi anakaribishwa kutembelea eneo la Bandari ya Nchi Kavu - Ubungo ili kukagua mazao hayo ya misitu muda wa kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) alasiri siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu. Ukaguzi huo utafanyika kuanzia tarehe ya Tangazo hili hadi tarehe 28 Machi, 2021. Aidha, Maafisa Misitu wa Wakala watakuwepo kwa ajili ya kutoa maelezo ya ziada ikiwa yatahitajika.

4. Mnunuzi mwenye nia ya kushiriki mnada anatakiwa kuwasilisha kwenye bahasha iliyofungwa nia ya kushiriki mauzo kwa njia ya mnada akiainisha namba ya kontena na pendekezo la bei kwa meta moja ya ujazo anaotarajia kununua kwa kufuata orodha kwenye Jedwali namba 1 la Tangazo hili. Aidha, Jedwali hili litatumika kuchagua kotena lenye magogo ya kununua kwa kuzingatia taarifa zilizoorodheshwa kama ifuatavyo: -

## JEDWALI Na. 1: ORODHA YA KONTENA YENYE MAGOGO KATIKA BANDARI YA NCHI KAVU - UBUNGO

| Na. | Namba ya Kontena | Idadi ya magogo kwa Kontena | Meta za ujazo kwa Kontena ($M^3$) | Bei ya kuanzia kwa kila meta ya ujazo (TZS/$M^3$) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | TEMU 6485178 | 178 | 22.093 | 1,209,637.80 |
| 2. | TCNU 9256750 | 291 | 23.196 | 1,200,999.90 |
| 3. | MSKU 8582963 | 484 | 23.5172 | 1,198,660.50 |
| 4. | MRKU 4642487 | 254 | 22.510 | 1,206,253.70 |
| 5. | TCKU 9652865 | 362 | 20.043 | 1,228,141.95 |
| 6. | MRKU 4189046 | 234 | 25.714 | 1,184,120.10 |
| 7. | MRKU 0882089 | 339 | 22.392 | 1,207,221.00 |
| 8. | PONU 1735037 | 341 | 23.226 | 1,200,798.10 |
| 9. | MSKU 6966189 | 299 | 25.075 | 1,188,111.60 |
| 10. | BMOU 4384225 | 258 | 24.5755 | 1,191,333.10 |
| 11. | MRKU 0470081 | 345 | 31.707 | 1,154,721.30 |
| 12. | MSKU 6260720 | 286 | 25.217 | 1,187,206.35 |
| 13. | MSKU 6162750 | 344 | 25.075 | 1,107,648.50 |
| 14. | MSKU 6257481 | 254 | 20.082 | 1,227,763.00 |
| 15. | PCIU 8894122 | 440 | 24.403 | 1,192,483.70 |
| 16. | MRKU 0498330 | 273 | 23.898 | 1,195,950.20 |
| 17. | MRKU 4670133 | 360 | 33.392 | 1,148,350.00 |
| 18. | MRKU 0761976 | 277 | 29.435 | 1,164,468.40 |
| 19. | PCIU 8199774 | 279 | 25.198 | 1,187,330.00 |
| 20. | MSKU 6162679 | 327 | 21.780 | 1,212,223.80 |
| 21. | TCLU 1482369 | 275 | 21.178 | 1,217,449.30 |
| 22. | GLDU 7462085 | 364 | 23.547 | 1,198,448.85 |
| 23. | MAEU 6203471 | 288 | 23.283 | 1,200,348.55 |
| 24. | PCIU 8331520 | 297 | 21.572 | 1,213,984.30 |
| 25. | TGHU 9472406 | 376 | 25.493 | 1,185,489.70 |
| 26. | PONU 7529326 | 330 | 29.445 | 1,164,410.50 |
| 27. | CMAU 5815607 | 282 | 24.190 | 1,193,914.80 |
| 28. | PCIU 8574690 | 223 | 21.299 | 1,216,354.60 |
| 29. | TGHU 8691858 | 435 | 25.194 | 1,187,351.35 |
| 30. | MRKU 4029963 | 343 | 27.691 | 1,173,009.70 |
| 31. | AAAU 4000216 | 264 | 21.272 | 1,216,590.70 |
| 32. | MSKU 9574290 | 372 | 27.252 | 1,175,350.30 |
| 33. | EISU 9386912 | 277 | 19.992 | 1,228,657.40 |
| 34. | MSKU 0129740 | 284 | 18.568 | 1,244,015.00 |
| 35. | MRKU 3664012 | 241 | 17.359 | 1,259,016.00 |
| 36. | MSKU 1555755 | 274 | 25.552 | 1,185,129.60 |
| 37. | TGHU 7623118 | 431 | 26.465 | 1,179,704.95 |
| 38. | MIEU 0057381 | 273 | 24.860 | 847,869.40 |
| 39. | CBHU 8497894 | 251 | 24.284 | 1,193,302.60 |

| Na. | Namba ya Kontena | Idadi ya magogo kwa Kontena | Meta za ujazo kwa Kontena ($M^3$) | Bei ya kuanzia kwa kila meta ya ujazo (TZS/$M^3$) |
|---|---|---|---|---|
| 40. | MSKU 8023815 | 73 | 6.508 | 1,643,239.85 |
| 41. | MRKU 2080930 | 262 | 15.958 | 1,279,251.40 |
| 42. | MSKU 0516727 | 305 | 19.437 | 1,234,355.80 |
| 43. | PCIU 8027409 | 216 | 12.134 | 1,358,234.00 |
| 44. | PONU 7389564 | 356 | 16.604 | 1,269,455.20 |
| 45. | TCLU 5958026 | 449 | 24.746 | 1,190,228.45 |
| 46. | MRKU 5458915 | 528 | 19.938 | 1,229,213.35 |
| 47. | MSKU 9035410 | 465 | 27.276 | 1,175,205.10 |
| 48. | MRKU 4392881 | 306 | 25.888 | 1,183,089.40 |
| 49. | CLHU 8931911 | 197 | 18.872 | 1,240,544.20 |
| 50. | GESU 5044285 | 324 | 20.412 | 1,224,522.70 |
| 51. | MRKU 2389791 | 238 | 23.832 | 1,196,409.00 |
| 52. | PONU 7934524 | 312 | 24.078 | 1,194,714.60 |
| 53. | MSKU 0377941 | 262 | 16.945 | 1,264,616.50 |
| 54. | INKU 2224640 | 263 | 22.111 | 1,209,489.20 |
| 55. | TCNU 8495914 | 420 | 28.934 | 1,166,826.20 |
| 56. | UESU 4122258 | 278 | 20.682 | 1,221,971.10 |
| 57. | MSKU 8710323 | 357 | 21.681 | 1,213,042.20 |
| 58. | PCIU 8910373 | 485 | 27.578 | 1,173,632.80 |
| 59. | MSKU 1869709 | 288 | 22.387 | 1,207,258.30 |
| | **Jumla** | **18,489** | **1,357.026** | |

5. Idadi ya magogo kwa kila kontena itanadiwa peke yake kulingana na bei na ujazo uliopo. Hata hivyo, bei ya juu itakayotolewa na mnunuzi mshiriki wakati wa kufungua bahasha ndiyo itakuwa bei ya kuanzia kunadi kila meta moja ya ujazo kwa kontena na bei hiyo haitazuia wanunuzi wengine kuongeza bei zao wakati wa mnada.

6. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania utatoa barua ya ushindi kwa mnunuzi aliyeshinda mnada kwa kila Kontena.

7. Mnunuzi atakayeshinda atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25 %) ya thamani yote ya ununuzi ndani ya siku tatu (3) za kazi kuanzia siku ya mnada. Fedha hizo hazitarudishwa endapo mshindi atashindwa kulipia ujazo wote aliouziwa. Asilimia sabini na tano (75 %) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia siku ya mnada. Malipo yote yafanyike kupitia benki au mitandao ya watoa huduma za kifedha baada ya kupewa hati ya madai (bill) kutoka Mfumo wa Makusanyo ya Serikali (GePG) itakayotolewa na Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu (TFS).

8. Mnunuzi aliyeshinda atapaswa kuwasilisha hati ya malipo (pay-in-slip) kwa mkuu wa kitengo cha Leseni cha Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kama uthibitisho wa malipo na siyo zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.

9. Mnunuzi aliyeshinda mnada atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kumaliza kulipa malipo yote kwa asilimia 100.

10. Mnunuzi aliyeshinda atatakiwa kuzingatia Sheria ya Misitu Sura 323 na Kanuni zake za Mwaka 2004 zinazohusiana na kufanya biashara ya mazao ya misitu na kusafirisha magogo nje ya nchi kabla ya kuanza kuondoa mazao ya misitu aliyonunua.

11. Usajili wa wanunuzi wenye nia ya kununua na watazamaji utafanyika Bandari ya Nchi Kavu - Ubungo kuanzia saa moja na nusu (1:30) asubuhi hadi saa nne kamili (4:00) asubuhi siku ya mnada. Aidha, wanunuzi watakaochelewa kuwasilisha nia zao kwa siku na muda uliopangwa hawataruhusiwa kushiriki katika mnada.

12. Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti zifuatazo za: www.tfs.go.tz na www.mnrt.go.tz.

Limetolewa na

**MTENDAJI MKUU**
**S. L. P 40832**
**DAR ES SALAAM**